MAKALA TANO MAARUFU ZA MWENYEKITI MAO



WAFANYAKAZI WA DUNIA NZIMA UNGANENI!

MAKALA TANO MAARUFU ZA MWENYEKITI MAO



OFISI YA UCHAPAJI
WA LUGHA ZA KIGENI
PEKING 1972

Kitabu cha Mfukoni

MAELEZO YA MPIGA CHAPA

Tafsiri hii ya Kiswahili ya *Makala Tano Maarufu za Mwenyekiti Mao* imefanywa kutokana na kitabu cha lugha ya Kichina ambacho kimepigwa chapa na Jumba la Uchapaji la Umma, Peking, mnamo Desemba 1967.

Kimepigwa chapa katika Jamburi ya Watu wa China



毛澤东

YALIYOMO

TUMIKIA UMMA 1

KWA AJILI YA UKUMBUSHO WA NORMAN BETHUNE 6

MZEE YU KONG ALIYEIONDOSHA MILIMA 13

JUU YA KUSAHIHISHA MAWAZO YA MAKOSA KATIKA CHAMA 24

Juu ya Maoni ya Kujali Mambo ya Kijeshi tu 26

Juu ya Demokrasi ya Kupindukia Mpaka 34

Juu ya Maoni ya Kutojali Nidhamu ya Oganaizeshen 39

Juu ya Mawazo ya Usawa wa Kupindukia Mpaka 42
Juu ya Mawazo ya *Subjective* 46
Juu ya Ubinafsi 49
Juu ya Mawazo ya Vikosi vya Kiharamia vya Kuzurura Zurura 54
Juu ya Masalio ya *Putschism* 58

YAPINGE MAWAZO YA KILIBERALI 60

TUMIKIA UMMA

Septemba 8, 1944

Chama chetu cha Kikoministi pamoja na majeshi yanayoongozwa na Chama chetu — Jeshi la Njia ya Nane na Jeshi Jipya la Nne — ni vikosi vya kimapinduzi. Vikosi vyetu hivi vimejisabilia moja kwa moja kwa ajili ya ukombozi wa umma na kutumikia kwa ukamilifu maslaha ya umma. Komredi Chang Szu-teh alikuwemo katika vikosi hivi.

Watu wote lazima kufa, lakini kifo kinaweza kubadilika katika umuhimu wake. Mwandishi wa zamani wa Kichina, Szuma Chien, alisema: "Ingawa kifo kinawaangukia watu wote

sawasawa, lakini kinaweza kuwa kizito kuliko Mlima wa Tai au kuwa chepesi kuliko unyoya." Kufa kwa ajili ya maslaha ya umma ni jambo zito kuliko Mlima wa Tai, lakini kufanya kazi kwa ajili ya mafashisti na kufa kwa ajili ya wanyonyaji damu na wakandamizi ni kitu chepesi kuliko unyoya. Komredi Chang Szu-teh amekufa kwa ajili ya maslaha ya umma, na kifo chake ni kizito kuliko Mlima wa Tai.

Ikiwa tunao upungufu, hatuogopi kuonyeshwa na kutolewa makosa, kwa sababu sisi tunatumikia umma. Mtu ye yote — bila ya kujali mtu gani — anaweza kutuonyesha makosa yetu, na ikiwa jambo analolisema ni barabara basi tutayasahihisha makosa hayo. Ikiwa jambo analotoa shauri ni lenye manufaa kwa umma,

basi shauri lake tutalifuata. Shauri la "vikosi bora na kurahisisha kazi za utawala" lilitolewa na Bwana Li Ting-ming, ambaye si Mkoministi; lakini alitoa shauri zuri lenye manufaa kwa umma, na kwa hivyo tumelifuata. Ikiwa kwa ajili ya maslaha ya umma, tutashikilia kulifanya jambo lililo barabara na kulisahihisha lililo la makosa, basi bila ya shaka yo yote vikosi vyetu hivi vitasitawi.

Sisi tunatoka pande mbali mbali za nchini na tumeungana pamoja kwa ajili ya lengo la pamoja la mapinduzi. Na tunahitajia aktharia ya umma kuwa pamoja nasi katika kwendea kwenye lengo hili. Leo tumeshakuwa tunaongoza maeneo ya vituo yenye watu milioni 91, lakini bado hayatoshi, bado inahitaji maeneo makubwa zaidi, na hiyo tu tutaweza ku-

likomboa taifa lote. Katika wakati wa shida, sisi makomredi tusiyasahau mafanikio yetu, lazima tuuone mustakbala mzuri ulio mbele yetu na tuwe na ushujaa zaidi. Watu wa China wamo katika dhiki; ni wajibu wetu kuwaokoa, na lazima tupigane kwa juhudi. Kila penye jihadi, kuna kujitolea mhanga, na kifo ni matokeo ya kidesturi. Lakini maslaha ya umma na dhiki za wingi mkubwa wa umma ziko nyoyoni mwetu, na tunapokufa kwa ajili ya umma kinakuwa kifo thamini. Hata hivyo, lazima tujitahidi kama iwezekanavyo kuepusha kujitolea mhanga kusiko lazima. Maofisa wetu lazima wamshughulikie kila askari, na watu wote miongoni mwa vikosi vya kimapinduzi lazima wafikiriane, watendeane wema na wasaidiane.

Tokea hivi sasa atakapokufa ye yote miongoni mwa vikosi vyetu ambaye kafanya kazi ya manufaa, inatuwajibikia tufanye mazishi ya heshima pamoja na mkutano wa ukumbusho wa marehemu — ikiwa mtu huyo ni mpishi au askari. Jambo hili liwe ni kanuni. Na lienezwe miongoni mwa umma vile vile. Anapokufa mtu katika kijiji, mkutano wa kumkumbuka marehemu unafalia ufanywe. Kwa njia hii, tutaeleza huzuni zetu kwa kifo cha mtu huyo pamoja na kuunganisha umma wote.

KWA AJILI YA UKUMBUSHO WA NORMAN BETHUNE

Desemba 21, 1939

Komredi Norman Bethune, mwanachama wa Chama cha Kikoministi cha Canada, alikuwa na umri wa zaidi ya miaka 50 wakati alipopelekwa na Vyama vya Kikoministi vya Canada na Marekani kuja China; yeye hakulifikiria kama ni jambo zito kwake kusafiri masafa ya maelfu ya maili kuja kutusaidia katika Vita vya Kupinga Japani. Alifika Yenan katika majira ya *spring* mwaka jana, baadaye alikwenda kufanya kazi katika Mlima wa Wutai na — kwa masikitiko yetu makubwa — alijitolea mai-

sha katika kuifanya kazi yake. Jee huu ni moyo wa namna gani uliomfanya mtu wa nchi nyengine kutojifikiria binafsi na kuifanya jihadi ya ukombozi wa watu wa China kama ni jihadi yake mwenyewe? Huu ni moyo wa udugu wa kilimwengu, na wa kikoministi — jambo ambalo linamwajibikia kila mwanachama wa Chama cha Kikoministi cha China ajifunze. Ulenin unafikiria kwamba mapinduzi ya dunia yanaweza kufanikiwa pindi tu ikiwa tabaka la kifanyakazi la nchi za kibepari launga mkono jihadi ya ukombozi ya watu katika makoloni na nusu-makoloni, na ikiwa tabaka la kifanyakazi katika makoloni na nusu-makoloni launga mkono jihadi ya ukombozi ya tabaka la kifanyakazi la nchi za kibepari. Komredi Bethune aliufuata

msimamo huu wa Ulenin kwa vitendo hasa. Ni lazima sisi wanachama wa Chama cha Kikoministi cha China pia tuufuate msimamo huu katika vitendo vyetu. Inatupasa tuungane na tabaka la kifanyakazi la nchi zote za kibepari: tuungane na tabaka la kifanyakazi la Japani, Uingereza, Marekani, Ujarumani, Utaliana na la nchi zote nyenginezo za kibepari, na hapo ndio patawezekana kuuangamiza ubeberu, kukomboa taifa na umma wetu, na kukomboa mataifa na watu wengineo wa dunia. Huu ndio udugu wetu wa kilimwengu, udugu wa kilimwengu tunaoutumia katika kuupinga uwananchi mbovu wa mtu kupendelea taifa lake na nchi yake tu.

Moyo wa Komredi Bethune wa kujisabilia moja kwa moja katika kuwatumikia watu wengine, bila ya

kujifikiria binafsi hata chembe, ulionekana wazi wazi kwa jinsi alivyokuwa akiifanya kazi yake kwa madaraka makubwa kabisa na ukunjufu wake mkubwa kabisa kwa makomredi na umma. Kila Mkoministi lazima ajifunze kutoka kwake. Wako watu kadha wasio na tabia ya madaraka katika kazi yao, wanapendelea kazi nyepesi na kuikimbia kazi nzito, wanawatupia wenzao mizigo mizito na wao wenyewe kujichagulia iliyo mepesi. Katika kila kitu, wanajifikiria binafsi kabla ya kuwafikiria wengine. Wanapoifanya kazi ndogo ya manufaa, mara hujaa majivuno na hujigamba kila waendapo kwa kuogopea watu wengine hawatojua. Watu wa namna hiyo hawana ukunjufu, huruma, ni watepetevu na hawawajali makomredi na umma. Kusema kweli,

watu kama hao si Makoministi au kwa uchache hawawezi kuhesabiwa kama ni Makoministi wa kikweli kweli. Hapana ye yote aliyetoka kwenye medani ambaye hakuzieleza sifa za Bethune, na po pote linapotajwa jina lake hapana asiyevutika na namna alivyojisabilia. Katika eneo la mpaka la Shansi-Chahar-Hopei, hapana mwanajeshi au raia aliyetibiwa na Daktari Bethune au kuona bidii zake ambaye hakuvutika na juhudi zake. Kila Mkoministi lazima ajifunze moyo wa kikoministi wa kikweli kutokana na Komredi Bethune.

Komredi Bethune alikuwa ni daktari, kutibu watu ndio kazi yake, na kila kukicha alikuwa akiuinua ustadi wake — ustadi ambao ulikuwa wa daraja ya juu sana miongoni mwa madaktari wa Jeshi la Njia ya Nane.

Mfano wa Komredi Bethune ni somo kubwa kwa wale watakao kubadilisha kazi zao mara wanapoona mambo yamebadilika na kwa wale wanaozidharau kazi za ufundi kwa kuzifikiria hazina faida wala mustakbala wo wote mzuri.

Komredi Bethune na mimi tumekutana mara moja tu. Baadaye aliniandikia barua nyingi. Lakini mimi nilimwandikia barua moja tu kwa vile nilivyokuwa nimeshughulika — barua ambayo sijui ilimfika au la. Nina huzuni kubwa juu ya kifo chake. Sasa sote tumo kumkumbuka, jambo ambalo laonyesha kwamba sote tumevutika kwa moyo wake. Lazima sote tujifunze kutokana na moyo wake wa kutojifikiria binafsi hata chembe. Na pindi tukiwa na moyo kama huu, basi kila mmoja atakuwa ni mtu wa

manufaa kwa umma. Uwezo wa mtu unaweza kuwa mkubwa au mdogo, lakini akiwa na moyo kama huu, mtu huyo keshakuwa mtu mwenye mawazo matukufu na msafi, mtu wa heshima, mtu asiyeshughulikia mambo ya upuuzi upuuzi na mtu wa manufaa kwa umma.

MZEE YU KONG ALIYEIONDOSHA MILIMA

Juni 11, 1945

Mkutano wetu umefanikiwa sana. Tumeyafanya mambo matatu. Kwanza, tumekata shauri juu ya msimamo wa Chama — yaani kwa ushujaa kuwaamsha umma na kuzipanua nguvu za umma ili, kwa kufuata uongozi wa Chama chetu, ziweze kuwashinda washambulizi wa Kijapani, kuwakomboa watu wa nchini kote na kuijenga China ya udemokrasi mpya. Pili, tumeipasisha Katiba mpya ya Chama. Tatu, tumeichagua idara ya uongozi wa Chama, yaani Kamiti Kuu. Kwa hivyo, kazi yetu

ya tangu leo ni kukiongoza Chama kizima katika kuutekeleza msimamo wa Chama. Mkutano wetu umekuwa mkutano wa ushindi, mkutano wa umoja. Wajumbe wametoa maoni mazuri sana kuhusu ripoti tatu. Makomredi wengi walijitoa makosa kwa kufanya umoja kama ni lengo lao, na kwa hivyo tumefikia kwenye umoja kwa njia ya kujitoa makosa. Mkutano huu ni mfano wa umoja, mfano wa kujitoa makosa, mfano wa demokrasi ndani ya Chama.

Baada ya mkutano mkuu kufungwa, makomredi wengi watarejea kwenye kazi zao mbali mbali na kwenye medani mbali mbali za vita. Makomredi, po pote mtapokwenda inakuwajibikieni kuueneza msimamo wa mkutano huu na, kwa kupitia makom-

redi wote wa Chama, kuwaeleza umma kwa kiwango kikubwa.

Madhumuni yetu katika kuueneza msimamo wa mkutano huu ni kutaka kufanya Chama kizima na umma wa nchi nzima kuwa na imani juu ya ushindi usio na shaka wa mapinduzi. Mwanzo ni lazima kukifanya kikosi cha watangulizi wainue juu ufahamu wao wa kisiasa ili wawe imara, wasiogope kujitolea mhanga, wazivuke kila shida na wajipatie ushindi. Lakini jambo hili halitoshi; ni lazima vile vile kuwafanya umma mkubwa nchini kote wainue ufahamu wa kisiasa ili, kwa hiari zao na kwa furaha, washirikiane pamoja nasi katika kupigania ushindi. Lazima tuwafanye umma waamini kuwa China si ya wapinga maendeleo bali ni ya umma wa China. Iko hekaya ya kale ya Ki-

china iitwayo "Mzee Yu Kong Aliyeiondosha Milima". Hadithi hii yasimulia juu ya kizee aliyekuwa akiishi katika kaskazini ya China zamani sana ambaye alikuwa akiitwa Mzee Yu Kong wa Mlima wa Kaskazini. Nyumba yake ilikuwa ikikabili upande wa kusini, na karibu na mlango wake palikuweko milima miwili mikubwa—Taihang na Wangwu — ambayo ilikuwa ikiziba njia. Mzee Yu Kong aliwaongoza watoto wake wanaume na, kwa azma kubwa, wakaanza kuichimba milima hiyo kwa kutumia jembe. Kizee mwengine — ajulikanaye kama Mzee Mwerevu — aliwaona wakifanya hivyo na kwa msemo wa dharau akawaambia, "Upumbavu gani mlionao kwa kufanya jambo hili! Ni muhali kwa nyinyi watu wachache kuweza kui-

chimba milima hii miwili mikubwa." Mzee Yu Kong akajibu, "Nitapokufa, watoto wangu wataendelea; watapokufa wao, wajukuu wangu wataendelea; watapokufa wajukuu wangu, virembwe vyangu vitaendelea na kadhalika. Milima hii ingawa ni mirefu, lakini haiwezi kuwa mirefu kuliko hivi ilivyo na kila kipande kidogo cha mlima tutakapokiondosha basi mlima utakuwa mfupi na mfupi zaidi. Kwa nini tusiweze kuiondosha milima hii?" Baada ya kuyapinga mawazo ya makosa ya Mzee Mwerevu, Mzee Yu Kong akaendelea kila siku kuichimba milima hiyo bila ya kutikisika imani yake. Mungu akavutiwa na jambo hilo, na akawapeleka duniani malaika wawili kuichukua milima hiyo juu ya mabega yao. Hivi leo iko milima miwili mikubwa iliyouelemea umma

wa China. Mlima mmoja ni ubeberu na wa pili ni umwinyi. Chama cha Kikoministi cha China tokea zamani kimeazimia kuiondosha milima hii. Lazima tuwe wastahamilivu na tufanye kazi bila ya kusita, na sisi vile vile tumfanye Mungu avutike. Mungu wetu si ye yote isipokuwa ni umma mkubwa wa China nzima. Ikiwa umma watavinjari na kushirikiana nasi katika kuichimba milima hii, kwa nini tusiweze kuiondosha?

Jana nilipokuwa nikizungumza na Wamarekani wawili waliokuwa wakienda Marekani, niliwaambia kwamba serikali ya Marekani yajaribu kutufisidi lakini jambo hilo hatuliruhusu. Sisi tunaipinga siasa ya serikali ya Kimarekani ya kumuunga mkono Chiang Kai-shek katika kuwapinga Makoministi. Lakini ni lazima

tuweke mpambanuo, kwanza, baina ya watu wa Marekani na serikali yao na, pili, baina ya watengezaji siasa wa serikali ya Kimarekani na watumishi walio chini yao. Niliwaambia Wamarekani hao wawili kuwa "waambieni watengezaji siasa wa serikali yenu ya Kimarekani kwamba hatukuruhusuni nyinyi kuingia katika Maeneo Yaliyokombolewa kwa sababu siasa yenu ni ya kumuunga mkono Chiang Kai-shek dhidi ya Makoministi, na kwa hivyo lazima sisi tujihadhari. Mnaweza kuja katika Maeneo Yaliyokombolewa ikiwa madhumuni yenu ni kushiriki katika mapigano dhidi ya Japani, lakini mwanzo lazima paweko makubaliano. Hatutokuruhusuni kuzurura kisiri siri kila mwahala. Ilivyokuwa Patrick J. Hurley katangaza wazi wazi kupinga mashirikiano na Chama

cha Kikoministi cha China, basi kwa nini bado mnataka kuja katika Maeneo yetu Yaliyokombolewa na kuzurura?"

Siasa ya serikali ya Kimarekani ya kumuunga mkono Chiang Kai-shek katika kuwapinga Makoministi yaonyesha wazimu wa wapinga maendeleo wa Kimarekani. Lakini majungu yote ya wapinga maendeleo wa kigeni au wa Kichina ya kuzuia ushindi wa umma wa China bila ya shaka yo yote yatashindwa. Nguvu za kidemokrasi ndio mkondo mkuu katika dunia ya leo, na upingaji maendeleo ulio dhidi ya demokrasi ni mkondo uendao kinyume tu. Hivi sasa mkondo wa upingaji maendeleo umo kujaribu kuuangamiza mkondo mkuu wa uhuru wa kitaifa na demokrasi ya umma, lakini milele hautoweza kuwa mkondo

mkuu. Leo bado iko mivutano mitatu mikubwa katika dunia kongwe, kama vile alivyoitaja Stalin muda mrefu uliopita. Mivutano hiyo ni: kwanza, mvutano baina ya tabaka la kifanyakazi na tabaka la kibepari katika nchi za kibeberu; pili, mvutano baina ya madola mbali mbali ya kibeberu; na tatu, mvutano baina ya nchi zilizo makoloni na nusu-makoloni kwa upande mmoja, na nchi za kibeberu zinazotawala makoloni kwa upande wa pili. Si kama mivutano hii mitatu inaendelea tu bali vile vile imekuwa mikali zaidi na kuenea zaidi kila kukicha. Kwa sababu ya kuweko na kukua mivutano hii, basi utakuja wakati ambapo mkondo uendao kinyume wa upingaji maendeleo — wa kupinga Soviet Union, kupinga Ukoministi na kupinga demokrasi —utafyekwa.

Katika wakati huu iko mikutano miwili mikuu ifanywao katika China — Mkutano Mkuu wa Sita wa Kitaifa wa Wajumbe wa Kuomintang na Mkutano Mkuu wa Saba wa Kitaifa wa Wajumbe wa Chama cha Kikoministi. Mikutano hii miwili ina madhumuni tofauti kabisa: madhumuni ya mkutano mmoja ni kukifyeka Chama cha Kikoministi na nguvu zote nyenginezo za kidemokrasi katika China na kuitia China katika kiza; madhumuni ya mkutano mwengine ni kuupindua ubeberu wa Kijapani na vibaraka vyake, yaani nguvu za kimwinyi za Kichina, na kuijenga China ya udemokrasi mpya na kwa hivyo kuiongoza China iendee kwenye mwangaza. Misimamo hii miwili inapingana. Tunaamini kwa udhati kwamba umma wa China —

kwa kufuata uongozi wa Chama cha Kikoministi cha China na msimamo wa Mkutano wake Mkuu wa Saba — utajipatia ushindi uliokamilika, na msimamo wa kipinga mapinduzi wa ki-Kuomintang bila ya muepuko wo wote utashindwa.

JUU YA KUSAHIHISHA MAWAZO YA MAKOSA KATIKA CHAMA

Desemba, 1929

Yako mawazo mbali mbali yasiyo ya kifanyakazi katika oganaizeshen za Chama zilizoko kwenye Jeshi la Nne la Jeshi Jekundu ambayo yanazuia sana kutekelezwa msimamo sahihi wa Chama. Bila ya kuyasahihisha kwa ukamilifu mawazo hayo, Jeshi la Nne la Jeshi Jekundu halitoweza kabisa kubeba majukumu yake katika mapigano makubwa ya kimapinduzi ya China. Mzizi wa mawazo kama hayo ya makosa katika oganaizeshen

za Chama za Jeshi la Nne bila ya shaka uko katika oganaizeshen zake za msingi ambamo kwa wingi mkubwa wamo wakulima na watu wengine wenye asili ya mabepari wadogo; lakini juu ya hivyo, upungufu wa maidara ya uongozi ya Chama katika kufanya mapigano kwa pamoja na kwa uthabiti dhidi ya mawazo hayo yasiyo sahihi na kuwaelimisha wanachama wake juu ya msimamo sahihi wa Chama pia ni sababu muhimu ya kuweko na kukua kwake. Kwa mujibu wa moyo wa barua ya mwezi Septemba ya Kamiti Kuu, mkutano huu unaonyesha mimathilisho ya aina mbali mbali ya mawazo yasiyo ya kifanyakazi katika oganaizeshen za Chama za Jeshi la Nne, mizizi yake na njia za kuyasahihi-

sha, na unawatolea wito makomredi wote wayaondoshe kwa ukamilifu.

JUU YA MAONI YA KUJALI MAMBO YA KIJESHI TU

Maoni ya kujali mambo ya kijeshi tu yamekua sana miongoni mwa makomredi kadha katika Jeshi Jekundu. Maoni haya yanajionyesha kama hivi:

1. Makomredi hawa wanafikiria mambo ya kijeshi na kisiasa ni vitu vinavyopingana na wanakataa kukubali kwamba mambo ya kijeshi ni mojawapo tu katika njia za kutekeleza kazi za kisiasa. Baadhi yao hata wanasema "mkiwa mahodari katika mambo ya kijeshi, basi bila ya shaka mtakuwa mahodari katika mambo ya kisiasa; mkiwa si mahodari katika mambo ya kijeshi, basi hamwezi kuwa mahodari

katika mambo ya kisiasa" — hii ni kwenda hatua moja zaidi ya kuyapa mambo ya kijeshi uongozi juu ya mambo ya kisiasa.

2. Wao wanafikiria kwamba kazi ya Jeshi Jekundu, kama ile ya jeshi Jeupe, ni kupigana tu. Wao hawafahamu kwamba Jeshi Jekundu la China ni kundi lenye silaha la kutekeleza kazi za kisiasa za mapinduzi. Hasa katika wakati tulio nao, kazi za Jeshi Jekundu kabisa sio kupigana tu; mbali ya kupigana kuziangamiza nguvu za kijeshi za adui, lazima lichukue majukumu muhimu kama vile kufanya uenezi siasa miongoni mwa umma, kuwakusanya umma, kuwazatiti kwa silaha, na kuwasaidia kuanzisha hatamu za kiserikali za kimapinduzi na mpaka kuanzisha oganaizeshen za Chama. Jeshi Jekundu halipigani kwa

ajili ya kupigana tu, bali kwa sababu ya kufanya uenezi siasa miongoni mwa umma, kuwakusanya, kuwazatiti kwa silaha, na kuwasaidia kuanzisha hatamu za kiserikali za kimapinduzi. Bila ya malengo haya, basi mapigano yatapoteza maana yake na Jeshi Jekundu litapoteza madhumuni ya kuweko kwake.

3. Kwa hivyo, katika mambo ya oganaizeshen, makomredi hawa wanayafanya maidara ya Jeshi Jekundu yafanyayo kazi ya kisiasa kuwa chini ya yale yafanyayo kazi ya kijeshi, na wanatoa wito usemao "yawachie Makao Makuu ya Kijeshi kushughulikia mambo ya nje". Wazo hili likiwa litaachiwa kukua, litaleta hatari ya kutengana na umma, hatamu za kiserikali kudhibitiwa na jeshi na kutoka katika uongozi wa kifanyakazi — ita-

kuwa kuchukua njia ya ubwana-vita kama jeshi la Kuomintang lifanyavyo.

4. Kwa wakati huo huo, katika kazi ya uenezi siasa wao wameupuuza umuhimu wa vikundi vya uenezi siasa. Juu ya suala la jumuia za umma, wao wanapuuza kutengeza kamiti za maaskari katika jeshi na kuwakusanya pamoja umma wa wafanyakazi na wakulima wa kienyeji. Na matokeo ni kuwa kazi ya uenezi siasa na ya kioganaizeshen zote ziliwachwa.

5. Wao huwa na majivuno wanaposhinda vitani na huvunjika moyo wanaposhindwa vitani.

6. *Departmentalism* — wao wanafikiria juu ya Jeshi la Nne tu na hawafahamu kuwa ni mojawapo ya kazi muhimu za Jeshi Jekundu kuwazatiti umma wa kienyeji kwa silaha. Haya

ni mawazo yaliyokuzwa vikubwa ya mtengano wa vikundi vidogo vidogo.

7. Wakiwa hawawezi kuona mbali kupindukia mazingira yao ya kiwango fulani tu ya Jeshi la Nne, makomredi wachache wanaamini hapana nguvu yo yote nyengineyo ya kimapinduzi iliyoko. Na kwa hivyo, wao hupendelea kuliko kiasi wazo la kuhifadhi nguvu na kuepuka mapigano. Haya ni masalio ya uopotyunisti.

8. Baadhi ya makomredi, kwa kutofikiria hali za *subjective* na *objective*, wana ugonjwa wa papara papara katika kufanya mapinduzi; wao hawachukui juhudi kufanya kazi ndogo ndogo na ngumu miongoni mwa umma lakini kwa vile wamejaa mawazo ya ndoto, wanataka kufanya mambo makubwa makubwa tu. Haya ni masalio ya *putschism.*

Asili ya maoni ya kujali mambo ya kijeshi tu:

1. Daraja ndogo ya ufahamu wa kisiasa. Kutokana na jambo hili panakuja kutotambua jukumu la uongozi wa kisiasa katika jeshi na kutofahamu kuwa Jeshi Jekundu na jeshi Jeupe ni vitu tofauti kabisa.

2. Wazo la vikosi vya kuajiriwa. Maaskari wengi wa adui waliotekwa katika mapigano yaliyopita walijiunga katika Jeshi Jekundu, na watu kama hao wanakuja pamoja na mawazo ya kiwango kikubwa ya vikosi vya kuajiriwa, na kwa hivyo wanaleta katika daraja ya chini msingi wa maoni ya kujali mambo ya kijeshi tu.

3. Kutokana na sababu mbili zilizotajwa kabla panatokeza sababu ya tatu, yaani kuwa na imani ya kupindukia mpaka juu ya nguvu za kijeshi

na kutokuwa na imani juu ya nguvu za umma wa watu.

4. Chama kutoangalia na kutojadili kwa juhudi kazi ya kijeshi, pia ni sababu moja ya kuchomoza maoni ya kujali mambo ya kijeshi tu miongoni mwa makomredi kadha.

Njia za kusahihisha ni kama hizi zifuatazo:

1. Inua daraja ya ufahamu wa kisiasa katika Chama kwa njia ya elimu, ili kung'oa mizizi ya nadharia ya maoni ya kujali mambo ya kijeshi tu, na elewa kwa uwazi tofauti za msingi baina ya Jeshi Jekundu na jeshi Jeupe. Kwa wakati huo huo, ondosha masalio ya uopotyunisti na ya *putschism* na ivunje *departmentalism* ya Jeshi la Nne.

2. Engeza mafunzo ya kisiasa kwa maofisa na maaskari na hususan enge-

za elimu kwa wale ambao zamani walikuwa mateka. Kwa wakati huo, kama inavyoyumkinika, ziwaachie serikali za kienyeji kuteua wafanyakazi na wakulima wenye maarifa ya mapigano wajiunge katika Jeshi Jekundu, na kwa hivyo katika oganaizeshen yadhoofishwe na hata yaondoshwe kabisa maoni ya kujali mambo ya kijeshi tu.

3. Ziamshe oganaizeshen za kienyeji za Chama kutoa makosa oganaizeshen za Chama katika Jeshi Jekundu na yaamshe maidara ya hatamu za kiserikali kutoa makosa Jeshi Jekundu nafsi yake, kwa ajili ya kuleta taathira nzuri juu ya oganaizeshen za Chama za Jeshi Jekundu na maofisa na maaskari wake.

4. Chama lazima kwa bidii kishughulikie na kujadili kazi za kijeshi.

Kazi zote lazima zijadiliwe na zikatwe shauri na Chama kabla ya kutekelezwa na umma.

5. Tunga sheria na kanuni za Jeshi Jekundu ambazo zinaweka wazi kazi zake, mahusiano baina ya maidara yake ya kijeshi na ya kisiasa, mahusiano baina ya Jeshi Jekundu na umma wa watu na nguvu na kazi za kamiti za maaskari na mahusiano yake na maidara ya kijeshi na kisiasa.

JUU YA DEMOKRASI YA KUPINDUKIA MPAKA

Baada ya Jeshi la Nne la Jeshi Jekundu kukubali maelekezo ya Kamiti Kuu, imepungua vikubwa mimathilisho ya demokrasi ya kupindukia mpaka. Kwa mfano, maazimio ya Chama sasa yanatekelezwa kwa vizuri

kidogo; na hapana tena ye yote anayeleta madai ya makosa kama vile Jeshi Jekundu lazima lifuate "mpango wa demokrasi-uongozi kutoka chini mpaka juu" au "ziachie daraja za chini kujadili kwanza matatizo yote, na baadaye kuziwachia daraja za juu kukata shauri". Kusema kweli, kupungua huku ni jambo la muda tu la kijuujuu na haikusudii kuwa mawazo ya demokrasi ya kupindukia mpaka yameshaondoshwa kabisa. Kwa maneno mengine, mawazo ya demokrasi ya kupindukia mpaka bado yana mizizi mirefu katika akili za makomredi wengi. Hebu angalia mimathilisho ya namna kadha za kutekeleza bila ya hiari maazimio ya Chama.

Njia za kusahihisha ni kama zifuatavyo:

1. Katika mambo ya nadharia, ing'oe mizizi yote ya demokrasi ya kupindukia mpaka. Kwanza, ni lazima ionyeshwe kwamba demokrasi ya kupindukia mpaka ina hatari ya kutia hasara au hata kubomoa kabisa oganaizeshen za Chama na kudhoofisha na hata kupoteza kabisa uwezo wa kupigana wa Chama, na kukifanya Chama kisiweze kuchukua madaraka yake ya mapigano na kwa hivyo kuleta kushindwa kwa mapinduzi. Baada ya hapo, ni lazima ionyeshwe kuwa mizizi ya demokrasi ya kupindukia mpaka iko katika tabia ya mabepari wadogo ya kuikimbia nidhamu. Tabia hii inapoletwa katika Chama, basi hukua kuwa mawazo ya demokrasi ya kupindukia mpaka katika mambo ya siasa na oganaizeshen. Mawazo haya kabisa hayaambatani na

kazi za kimapigano za tabaka la kifanyakazi.

2. Katika mambo ya oganaizeshen, hakikisha maisha ya demokrasi chini ya maelekezo ya uongozi. Jambo hili lifanywe kwa namna hii:

(1) Maidara ya uongozi ya Chama lazima yatoe msimamo barabara wa uongozi na yalete matanzuo wakati matatizo yanapotokea, kwa ajili ya kujithibitisha kama ni viini vya uongozi.

(2) Maidara ya juu lazima yajue hali ya maidara ya chini na maisha ya umma kwa ajili ya kuwa na msingi wa *objective* wa kutoa uongozi sahihi.

(3) Maidara ya Chama katika daraja yo yote yasikate mashauri

ovyo ovyo katika kutanzua matatizo. Mara shauri linapokatwa, lazima litekelezwe kwa uthabiti.

(4) Maidara ya juu ya Chama yanapokwisha kata shauri lo lote muhimu lazima yayapelekee maidara ya chini na umma wa wanachama azimio lao bila ya kucheleewa. Njia yenyewe ni kuitisha mikutano ya wanaharakati au ya wanachama wa matawi ya Chama au hata wa safu (hali zinaporuhusu) na kuwatuma watu watoe ripoti katika mikutano hiyo.

(5) Maidara ya chini ya Chama na wanachama lazima wajadili kwa urefu maelekezo ya maidara ya juu ili kufahamu maana yake kwa ukamilifu na kukata shauri juu ya njia za kuyatekeleza.

JUU YA MAONI YA KUTOJALI NIDHAMU YA OGANAIZESHEN

Katika oganaizeshen za Chama za Jeshi la Nne, maoni ya kutojali nidhamu ya oganaizeshen yajionyesha kama hivi ifuatavyo:

A. Wachache kutowafuata walio wengi. Kwa mfano, wachache wanapoona shauri lao limekataliwa, basi hawatekelezi kwa udhati maazimio ya Chama.

Njia za kusahihisha ni kama zifuatazo:

1. Kwenye mikutano, wanaoshiriki wote washajiishwe kutoa maoni yao kwa ukamilifu kama inavyoyumkinika. Usahihi au makosa katika mabishano yo yote uwekwe wazi bila ya kuridhiana au kusitiriana. Kwa ajili

ya kufikilia uamuzi wazi kabisa, jambo lisiloweza kukatwa shauri katika mkutano mmoja lijadiliwe katika mkutano mwengine (pindi ikiwa hakutoizuia kazi).

2. Mojawapo ya nidhamu za Chama ni kuwa wachache wawafuate walio wengi. Ikiwa maoni ya wachache yamekataliwa, ni lazima waunge mkono azimio lililopasishwa na walio wengi. Ikiwa ni lazima, wao wanaweza kulileta jambo hilo kwenye mkutano ujao kwa ajili ya kujadiliwa tena, lakini mbali ya hivyo ni lazima kwa namna yo yote wasitende kinyume na azimio lililopasishwa.

B. Kutoa makosa bila ya kujali nidhamu ya oganaizeshen:

1. Utoaji makosa wa ndani ya Chama ni silaha ya kutilia nguvu oganaizeshen za Chama na kuengeza

uwezo wake wa kupigana. Lakini juu ya hivyo, katika oganaizeshen za Chama zilizoko kwenye Jeshi Jekundu, pengine utoaji makosa si kama hivyo, bali hugeuka kuwa mashambulizi kwa mtu binafsi. Matokeo ya kufanya hivyo yakawa ni kumdhuru mtu binafsi pamoja na oganaizeshen za Chama. Huu ni mmathilisho wa ubinafsi wa mabepari wadogo. Njia ya kusahihisha ni kuwasaidia wanachama kufahamu kuwa madhumuni ya kutoa makosa ni kuengeza uwezo wa kupigana wa Chama kwa ajili ya kupata ushindi katika mapigano ya kitabaka na usitumiwe kama ni chombo cha kufanyia mashambulizi kwa mtu binafsi.

2. Wanachama wengi hutoa makosa si ndani bali nje ya Chama. Sababu ni kuwa wanachama wa kawaida bado hawajafahamu vizuri umuhimu wa

oganaizeshen za Chama (mikutano yake na kadhalika), na hawaioni tofauti baina ya utoaji makosa wa ndani na nje ya Chama. Njia ya kusahihisha ni kuwaelimisha wanachama waufahamu umuhimu wa oganaizeshen za Chama na watoe makosa ya kamiti za Chama au ya makomredi kwenye mikutano ya Chama.

JUU YA MAWAZO YA USAWA WA KUPINDUKIA MPAKA

Mawazo ya usawa wa kupindukia mpaka yalikuwa yanaenea sana kwenye Jeshi Jekundu katika wakati fulani. Hii ni baadhi ya mifano. Kuhusu kuwapa pesa za matumizi maaskari waliojeruhiwa, palikuweko upinzani juu ya kupambanua waliojeruhiwa kidogo na sana, na yalitolewa

madai ya kupewa sawa kwa wote. Maofisa walipokuwa wakipanda farasi, ilikuwa ikifikiriwa kuwa jambo hilo si lazima kwa kazi zao bali ni alama ya kutokuweko usawa. Usawa wa kupindukia mpaka ulidaiwa katika kugawanya mahitajio ya maisha na palikuweko upinzani dhidi ya kutolewa mahitajio zaidi kwa zile idara zenye hali maalum. Juu ya ubebaji mchele, dai lilikuwa kwamba wote wabebe sawa, bila ya kujali umri au afya ya mtu. Usawa ulidaiwa katika kugawa vyumba vya kukaliwa kwa maaskari, na makao makuu yalikuwa yakitukanwa kwa kuchukua chumba kikubwa kidogo. Usawa ulidaiwa katika kupewa kazi, na palikuweko kutokubali kufanya kazi zaidi kidogo kuliko mwengine. Mawazo haya yalifika hadi hata palipokuweko watu

wawili waliojeruhiwa lakini iko machera moja tu, hapana mmoja aliyeweza kuchukuliwa kwa sababu hapana mmoja aliyekubali mwenzake aitumie kwanza. Mawazo ya usawa wa kupindukia mpaka, kama yanavyoonyeshwa na mifano hii, bado ni tatizo kubwa miongoni mwa maofisa na maaskari wa Jeshi Jekundu.

Mawazo ya usawa wa kupindukia mpaka, kama vile yalivyo mawazo ya demokrasi ya kupindukia mpaka katika mambo ya kisiasa, ni matokeo ya kazi za mikono na ya uchumi mdogo wa kilimo — tofauti ilioko tu ni kuwa aina moja yajionyesha katika maisha ya kisiasa na aina nyengine yajionyesha katika maisha ya kawaida.

Njia ya kusahihisha: Ni lazima tuonyeshe kwamba kabla ya kuon-

doshwa ubepari, usawa wa kupindukia mpaka ni ndoto tu ya wakulima na wamilikaji wadogo wadogo wengineo, na kwamba hata katika wakati wa usoshalisti hapawezi kuweko usawa wa kupindukia mpaka, kwani vitu vitagaiwa kwa kanuni ya "kutoka kila mmoja kwa mujibu wa uwezo wake, na kwa kila mmoja kwa mujibu wa kazi yake" pamoja na kufuata mahitajio ya kazi. Ugawaji wa vitu vya maisha katika Jeshi Jekundu ni lazima uwe na usawa kwa kiwango fulani, kama vile malipo sawa baina ya maofisa na maaskari, kwa sababu jambo hili linahitajika katika hali ya sasa ya mapigano. Lakini usawa wa kupindukia mpaka wa kutojali sababu yo yote lazima upingwe kwani jambo hilo halihitajiwi na mapigano; kinyume cha hivyo, linazuia mapigano.

JUU YA MAWAZO YA *SUBJECTIVE*

Mawazo ya *subjective* yako kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wanachama kadha, yakileta madhara makubwa katika kuchambua hali ya kisiasa na katika kuziongoza kazi. Sababu ni kuwa uchambuzi huo wa hali ya kisiasa na uongozaji wa kazi unaofanywa kwa mujibu wa mawazo ya *subjective* huleta matokeo ya uopotyunisti au *putschism*. Kuhusu utoaji makosa wa *subjective*, mazungumzo ya upuuzi na yasio na msingi au kutiliana shaka, mambo kama hayo ndani ya Chama mara nyingi huleta mizozano isio na msingi na kudhoofisha oganaizeshen za Chama.

Jambo jengine linalohitaji kutajwa lahusu utoaji makosa wa ndani ya

Chama nalo ni kwamba baadhi ya makomredi wanapuuza masuala muhimu na wanajishughulisha na masuala madogo madogo wakati wanapotoa makosa. Wao hawafahamu kwamba kazi muhimu ya utoaji makosa ni kutaja makosa ya kisiasa na ya kioganaizeshen. Kuhusu upungufu wa mtu binafsi, isipokuwa unapokuwa unahusiana na makosa ya kisiasa na oganaizeshen, hapana haja ya kutoa makosa sana na kuwafadhaisha makomredi wanaohusika. Zaidi ya hayo, mara utoaji makosa kama huo unapokua, basi iko hatari kubwa kuwa wanachama watajishughulisha sana juu ya makosa madogo madogo, na kila mmoja atakuwa mwoga na mwangalifu wa kupindukia mpaka na kusahau kazi za kisiasa za Chama.

Njia kuu ya kusahihisha ni kuwaelimisha wanachama ili tabia ya kisiasa na ya kisayansi iwe inaendesha fikra zao na maisha yao ya Chama. Kwa ajili ya kulifikilia lengo hili ni lazima: (1) kuwaelimisha wanachama watumie njia ya Umarx-lenin katika kuchambua hali ya kisiasa na kuzipima nguvu za kitabaka, badala ya kufanya uchambuzi na upimaji wa *subjective;* (2) kuyaelekeza maangalizi ya wanachama katika kuchungua na kusoma jamii na uchumi ili waweze kukata shauri juu ya mbinu za mapigano na njia za kufanya kazi, na kuwasaidia makomredi wafahamu kuwa bila ya kufanya uchunguzi wa hali hasa basi wataangukia kwenye shimo la mawazo ya ndoto na *putschism,* na (3) katika utoaji makosa wa ndani ya Chama, jihadhari na mambo ya *sub-*

jective, kukata shauri ovyo ovyo na utoaji makosa wa upuuzi; sema maneno yenye ushahidi thabiti na toa makosa kwa kutilia mkazo upande wa siasa.

JUU YA UBINAFSI

Muelekeo wa ubinafsi katika oganaizeshen za Chama zilizoko kwenye Jeshi Jekundu unajionyesha kama ifuatavyo:

1. Kulipiza kisasi. Baadhi ya makomredi, baada ya kutolewa makosa na komredi askari katika Chama, hutafuta fursa ya kumlipiza kisasi nje ya Chama, na njia mojawapo ni kumpiga au kumtukana komredi anayehusika. Wao vile vile hutafuta kulipiza kisasi ndani ya Chama. "Wewe umeniponda katika mkutano huu, kwa hivyo nitaangalia kujipatia njia fulani

ya kulipiza kisasi katika mkutano ujao." Kulipiza kisasi kama huko kwatokana na mazingatio ya kibinafsi tu, kwa kupuuza maslaha ya jumla ya tabaka na Chama. Shabaha yake si tabaka la uhasama, bali mtu binafsi miongoni mwetu wenyewe. Hili ni jambo la kuozesha na kudhoofisha oganaizeshen na uwezo wa kupigana wa Chama.

2. Mawazo ya "kujali kikundi kidogo tu". Baadhi ya makomredi wanafikiria maslaha ya kikundi chao kidogo tu na wanapuuza maslaha ya jumla. Ingawa kwa kijuujuu jambo hili halionyeshi kutafuta maslaha ya kibinafsi, lakini kusema kweli jambo hili ni mfano wa ubinafsi ulio bahili kabisa na pia una matokeo makubwa ya kuleta uharibifu na kutengana. Mawazo ya "kujali kikundi kidogo

tu" yalikuwa yamejaa katika Jeshi Jekundu, na ingawa pametokea maendeleo fulani baada ya kufanywa utoaji makosa, lakini bado yako masalio yake na juhudi zaidi zinatakikana kuyavuka.

3. Mawazo ya "kuajiriwa". Baadhi ya makomredi hawafahamu kwamba Chama na Jeshi Jekundu, ambao wao ni wanachama, ni vyombo vya kutekeleza kazi za mapinduzi. Wao hawatambui kwamba wao nafsi zao ndio wafanya mapinduzi, na wanafikiria dhamana yao iko kwa wakubwa wao tu na si kwa mapinduzi. Mawazo haya ya uregevu ya kufanya mapinduzi kwa kuajiriwa vile vile ni mmathilisho wa ubinafsi. Mawazo haya yanaeleza kwa nini hapana wanaharakati wengi wanaofanya kazi bila ya mashuruti kwa

ajili ya mapinduzi. Bila ya kufyekwa mawazo haya, idadi ya wanaharakati haitokua, na mzigo mzito wa mapinduzi utabakia juu ya mabega ya idadi ndogo ya watu, na kuleta hasara kubwa mno kwa mapigano.

4. Kutafuta anasa. Katika Jeshi Jekundu vile vile wako makomredi si wachache ambao ubinafsi wao unajionyesha katika kutafuta anasa. Siku zote wao hutumaini kwamba kikosi chao kitakwenda kwenye miji mikubwa. Wao wanataka kwenda huko si kwa ajili ya kufanya kazi bali kwa ajili ya kujistarehesha nafsi zao. Kitu wasichokipenda kabisa ni kufanya kazi katika maeneo Mekundu ambako maisha ni magumu.

5. Kutenda mambo kiregevu. Baadhi ya makomredi hutenda mambo kiregevu na husita kufanya kazi

zao wakati jambo lo lote linapokwenda kinyume na matakwa yao. Jambo hili latokana hasa na upungufu wa elimu, ingawa baadhi ya wakati vile vile latokana na waongozi kutofanya barabara katika kutanzua matatizo, kugawa kazi au kutekeleza nidhamu.

6. Tamaa ya kutoka jeshini. Idadi ya watu wanaoomba kutolewa jeshini kupelekwa katika kazi za kienyeji imo kuengezeka. Sababu ya jambo hili haitokani moja kwa moja na watu binafsi wenyewe tu bali pia yatokana na: (1) shida kubwa za kupita kiasi za vitu vya mahitajio ya maisha katika Jeshi Jekundu, (2) machofu baada ya mapigano marefu, na (3) waongozi kutofanya barabara katika kutanzua matatizo, kugawa kazi au kutekeleza nidhamu.

Njia kuu ya kusahihisha jambo hili ni kutilia nguvu elimu ili kuyasahihisha mawazo ya kibinafsi. Baadaye, ni kufanya barabara katika kutanzua matatizo, kugawa kazi na kutekeleza nidhamu. Zaidi ya hayo, ni lazima zitafutwe njia za kufanya bora maisha katika Jeshi Jekundu, na kila fursa itumiwe kwa ajili ya mapumziko na matengenezo ili kuinua hali ya maisha. Katika kazi yetu ya elimu ni lazima tueleze kuwa katika asili ya kijamii, ubinafsi ni mmathilisho wa mawazo ya mabepari wadogo na ya kibepari ndani ya Chama.

JUU YA MAWAZO YA VIKOSI VYA KIHARAMIA VYA KUZURURA ZURURA

Mawazo ya kisiasa ya vikosi vya kiharamia vya kuzurura zurura yame-

chomoza katika Jeshi Jekundu kwa sababu idadi ya watu wenye asili ya wazururaji ni kubwa na kwa sababu iko idadi kubwa ya wazururaji katika China, hususan katika majimbo mbali mbali ya kusini. Mawazo haya yanajionyesha kwa namna zifuatazo: (1) Baadhi ya watu wanataka kuengeza taathira yetu ya kisiasa kwa njia ya kufanya mapigano ya kigarila ya kuzurura zurura tu, lakini hawako tayari kuiengeza taathira hiyo kwa kufanya mapigano magumu ya kujenga maeneo ya vituo na kuanzisha hatamu za kiserikali za umma. (2) Katika kulipanua Jeshi Jekundu, baadhi ya watu wanafuata msimamo wa "kuajiri watu na kununua farasi" na "kuwaingiza ndani watoro na kuwakubali waasi" kuliko msimamo wa kupanua

Vikosi vya Walinzi Wekundu na Jeshi Jekundu la kienyeji na kwa hivyo kuzikuza nguvu kuu za Jeshi Jekundu. (3) Baadhi ya watu hawana ustahmilivu katika kufanya mapigano magumu kwa kushirikiana pamoja na umma, na wanataka tu kuenda kwenye miji mikubwa kwa ajili ya kula na kunywa na kutosheleza nyoyo zao. Mimathilisho yote hii ya mawazo ya kiharamia ya kuzurura zurura inazuia sana sana Jeshi Jekundu katika kufanya kazi zake zifaazo; na kwa hivyo kufyekwa kwake ni lengo muhimu katika mapigano ya kifikra ndani ya oganaizeshen za Chama zilizoko kwenye Jeshi Jekundu. Ni lazima ifahamike kwamba njia za kiharamia za kuzurura zurura za aina ya Huang Chao na Li Chuang haziruhusiwi katika hali ya sasa.

Njia za kusahihisha ni kama zifuatazo:

1. Engeza elimu, toa makosa mawazo yasio sahihi, na ondosha mawazo ya vikosi vya kiharamia vya kuzurura zurura.

2. Engeza elimu miongoni mwa sehemu za msingi za Jeshi Jekundu na miongoni mwa mateka walioingia jeshini karibuni ili kupinga mtizamo wa kihuni.

3. Waingize katika Jeshi Jekundu wafanyakazi na wakulima wenye bidii na maarifa ya mapigano ili kubadilisha asili yake.

4. Anzisha vikosi vipya vya Jeshi Jekundu kutokana miongoni mwa umma wa wafanyakazi na wakulima walio mapiganoni.

JUU YA MASALIO YA *PUTSCHISM*

Oganaizeshen za Chama katika Jeshi Jekundu zimeshafanya mapigano dhidi ya *putschism*, lakini si kwa kiwango kinachotosha. Kwa hivyo, masalio ya mawazo haya bado yako katika Jeshi Jekundu. Mimathilisho yake ni: (1) vitendo vya upofu bila ya kujali hali za *subjective* na za *objective*; (2) utekelezaji usiotosha na usio thabiti wa siasa za Chama kuhusu miji; (3) nidhamu ya kijeshi inarega rega, hususan katika wakati wa kushindwa; (4) vitendo vya kuunguza nyumba vifanywavyo na baadhi ya vikosi; na (5) vitendo vya kupiga risasi watoro na kutia adabu ya viboko, mambo yote mawili yakiwa ni maonyesho ya *putschism*. Katika asili yake ya kijamii, *putschism* ni mchan-

ganyiko wa mawazo ya wafanyakazi wazururaji na mabepari wadogo.

Njia za kusahihisha ni kama zifuatavyo:

1. Katika upande wa kifikra ondosha *putschism*.

2. Sahihisha vitendo vya *putschism* kwa sheria, kanuni na siasa.

YAPINGE MAWAZO YA KILIBERALI

Septemba 7, 1937

Sisi twapendelea kuifanya jihadi ya kifikra yenye msingi, kwa sababu hiyo ni silaha ya kuhakikisha umoja katika Chama cha Kikoministi na katika jumuia za kimapinduzi kwa ajili ya maslaha ya mapigano yetu. Kwa hivyo kila Mkoministi na kila mwanamapinduzi lazima aitumie silaha hii.

Lakini mawazo ya kiliberali yapinga jihadi ya kifikra na yataka amani isio na kanuni, na kwa hivyo huleta kuchomoza mtindo mbaya wa kushughulikia mambo ya upuuzi upuuzi na kupungua hisia za kimapinduzi na

kufanya baadhi ya oganaizeshen na watu waliomo katika Chama chetu na jumuia za kimapinduzi kupotoka kisiasa.

Mawazo ya kiliberali yajitokeza kwa namna nyingi.

Kuyawacha mambo yaende ovyo ovyo kwa ajili ya amani na urafiki katika wakati ambapo mtu kafanya makosa ya dhahiri na kutofanya mabishano ya kanuni kwa sababu mtu aliyefanya makosa ni mtu unayejuana naye tokea zamani, mtu wa mji mmoja naye, mmesoma shule pamoja au ni rafiki yako mkubwa, mpenzi wako, mwenzako wa kazini wa zamani au mfuasi wako wa zamani. Au kulitoa makosa jambo fulani kwa kijuujuu tu — badala ya kulisahihisha kikweli — kwa sababu ya kutoyaharibu maingiliano yako na mtu fulani. Matokeo

ni kwamba oganaizeshen pamoja na mtu anayehusika wote watadhurika. Hii ni aina ya kwanza ya mawazo ya kiliberali.

Kulitoa makosa jambo kwa njia isiyo ya madaraka katika mwahala pa faragha badala ya kupeleka kwa njia nzuri mashauri yako kwa oganaizeshen. Kutowaambia watu cho chote mbele ya uso wao na badala yake kunong'ona nong'ona nyuma ya migongo yao, au kutosema cho chote katika wakati wa mkutano na badala yake kunong'ona nong'ona baadaye. Kuonyesha kutoheshimu kanuni ya maisha ya pamoja na badala yake kufanya mambo kama unavyojitakia mwenyewe. Hii ni aina ya pili.

Kuyawacha mambo yajiendee ovyo ovyo maadam hayakuathiri wewe binafsi; kusema kidogo kama iwezeka-

navyo na ilhali unajua wazi makosa gani yaliyofanywa. Kuwa mwerevu na kutojitia "matatani" ili kujitafutia kuepuka lawama. Hii ni aina ya tatu.

Kutotii amri na badala yake kuwa na majivuno juu ya maoni yako. Kudai fursa maalum katika oganaizeshen lakini kupuuza nidhamu zake. Hii ni aina ya nne.

Kumshambulia mtu binafsi, kufanya ugomvi usio na maana kuzimwaga chuki zako za kibinafsi au kulipiza kisasi badala ya kufanya mabishano na jihadi dhidi ya mawazo yasiyo barabara kwa ajili ya umoja, maendeleo au kazi iweze kufanywa vizuri. Hii ni aina ya tano.

Kuyasikiliza maoni yasiyo barabara bila ya kuyapinga na hata kuyasikiliza maneno ya wapinga mapinduzi bila ya kuyaripoti, na badala yake kunya-

maa kimya kama hapana lo lote lililotokea. Hii ni aina ya sita.

Kutoeneza siasa ya Chama miongoni mwa umma, kutowashajiisha, kutosema cho chote mkutanoni kutofanya uchunguzi juu ya umma au kutowauliza hali zao na kutowajali na kutofanya jambo lo lote katika kutengeza maisha yao na kujisahau kama ni Mkoministi — yaani Mkoministi kujifanya kuwa sawa sawa na raia wa kidesturi. Hii ni aina ya saba.

Kumwona mtu akiyadhuru maslaha ya umma na bila ya kuhamaki, kutomnasihi asitishe vitendo vyake au kutomzuia au kutomfahamisha na badala yake kumwachia aendelee na vitendo vyake viovu. Hii ni aina ya nane.

Kutoutia moyo wako wote katika kazi na kufanya kazi bila ya mpango

au muelekeo maalum; kufanya kazi kwa uzembe na kwa kujipurukusha purukusha — "Maadam mtu ni mtawa basi ataendelea kupiga kengele ya hekalu." Hii ni aina ya tisa.

Kujifikiria kama umefanya kazi kubwa katika mapinduzi, kujivunia kama ni mtu mkubwa, kupuuza kazi ndogo ndogo na ilhali kazi kubwa huwezi kuzifanya, kufanya kazi ovyo ovyo na kutojitahidi katika kujifunza. Hii ni aina ya kumi.

Kufahamu makosa yako na ilhali hufanyi jambo lo lote katika kuyasahihisha makosa yako — yaani kuchukua tabia ya kiliberali kuhusu nafsi yako. Hii ni aina ya kumi na moja.

Ziko aina chungu nzima za mawazo ya kiliberali. Lakini aina hizi kumi na moja ndizo zilizo muhimu.

Mambo haya yote ni maonyesho ya mawazo ya kiliberali.

Mawazo ya kiliberali yana madhara makubwa kwa oganaizeshen za mkusanyiko wa kimapinduzi. Mawazo hayo kama kutu, yadhoofisha na kuharibu umoja, yasababisha kuharibika maingiliano na kufanya kazi kwa uregevu pamoja na kuleta kutosikilizana miongoni mwa makomredi. Mawazo haya yavifanya vikosi vya kimapinduzi visiungane sawa sawa, yaharibu nidhamu, yafanya siasa zisiweze kutekelezwa kikamilifu na yaleta mtengano baina ya oganaizeshen za Chama na umma wake. Huu ni mwendo mbaya sana.

Mawazo ya kiliberali yatokana na ubinafsi wa vibepari uchwara. Mawazo haya yaweka mbele kabisa maslaha ya mtu binafsi, na maslaha ya

mapinduzi kama ni jambo la pili. Na jambo hili huleta fikra, siasa na oganaizeshen kuwa ya kiliberali.

Watu wenye mawazo ya kiliberali wazifikiri kanuni za Umarx kama ni maneno ya vitabuni tu ya kikasuku yalio maanawi. Wao waukubali Umarx, lakini hawako tayari kuutekeleza, au hawako tayari kuutekeleza kwa ukamilifu, wao hawako tayari kuyatupa mawazo yao ya kiliberali na kuufuata kikweli Umarx. Watu hawa wanaufuata Umarx lakini, vile vile, wanayafuata mawazo ya kiliberali. Wao hubobozokwa juu ya Umarx lakini vitendo vyao ni vya mawazo ya kiliberali. Wao wautekeleza Umarx juu ya watu wengine lakini, kuhusu wao wenyewe, wayatekeleza mawazo ya kiliberali. Watu hawa wanazo bidhaa za namna mbili ambazo wazi-

tumia katika mambo mbali mbali. Hivyo ndivyo zinavyofanya kazi akili za baadhi ya watu.

Mawazo ya kiliberali ni mojawapo ya mimathilisho ya uopotyunisti, na ni kinyume kabisa na msingi wa Umarx. Mawazo ya kiliberali ni mawazo mabaya, mawazo ambayo hufanya kazi za kumsaidia adui. Na kwa sababu hii ndio maana adui apendelea mawazo ya kiliberali yaendelee kuweko miongoni mwetu. Ilivyokuwa tabia ya mawazo ya kiliberali ni ya namna hivi, basi inatulazimu tuyafyeke kabisa mawazo haya miongoni mwa wanamapinduzi.

Lazima tuutumie moyo wa kushajiisha wa Umarx katika kuyashinda mawazo ya kiliberali — mawazo ambayo ni mabaya sana. Mkoministi lazima awe kapanuka akili yake, mtiifu

na mtu imara na mwenye juhudi. Mkoministi, siku zote, lazima ayafikirie maslaha ya mapinduzi kama ni maisha yake hasa, na maslaha yake mwenyewe yawe chini ya maslaha ya mapinduzi. Mkoministi, siku zote na katika kila mwahala, inamwajibikia kufuata kanuni sahihi pamoja na kufanya jihadi bila ya kuchoka dhidi ya kila aina ya mawazo yasiyo sahihi na vitendo visivyo sahihi ili kuuimarisha msingi wa maisha ya pamoja ya Chama na kuyatilia nguvu maingiliano baina ya Chama na umma. Mkoministi lazima ajishughulishe na Chama na umma zaidi kuliko anavyoshughulikia binafsi mwenyewe; Mkoministi lazima awafikirie watu wengine zaidi kuliko anavyojifikiria mwenyewe. Ni kwa namna hivyo tu ndivyo ataweza kuwa Mkoministi wa kweli.

Makoministi wote walio watiifu, waaminifu, wenye juhudi na wa kweli lazima waungane katika kuupinga mwelekeo wa kiliberali unaoonekana katika baadhi ya watu walioko mion-goni mwetu ili kuwafanya watu hao waichukue njia iliyonyoka. Hii ni mojawapo katika kazi zinazotuwaji-bikia kuzifanya katika medani yetu ya fikra.

毛主席的五篇著作
*
外文出版社出版（北京）
1972年版
编号：（斯）1050—1541
00023
1—Sa—911Pk